


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**




**TAARIFA KWA UMMA**

**KUONGEZWA MUDA WA USAJILI WA NAMBA ZA SIMU ZA MKONONI**

1. Itakumbukwa kwamba Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa agizo kwamba namba zote za simu za mkononi (SIM Cards) zisajiliwe tangu tarehe 1 Julai, 2009 hadi tarehe 31 Desemba, 2009.
2. Sababu za kuanzisha utaratibu huu wa kusajili namba za simu (SIM Cards) zilielezwa katika mikutano mbalimbali na Wadau, ambazo zinajumuisha:-
  - (i) Kuwalinda watumiaji na matumizi mabaya ya huduma za mawasiliano.
  - (ii) Kuwezesha kuwatambua watumiaji wa huduma za ziada za simu, kama huduma za kibenki, kutuma na kupokea fedha, kufanya malipo mbalimbali kwa kutumia simu kwa mfano kulipia huduma za maji, umeme, vipindi vya televisheni vya kulipia nk.
  - (iii) Kuimalisha usalama wa taifa
  - (iv) Kuwawezesha watoa huduma za mawasiliano kuwafahamu vizuri wateja wao na kuwahudumia ipasavyo kadri ya mahitaji yao.
3. Kumekuwepo na mwitikio mkubwa kutoka kwa umma na watoa huduma za mawasiliano kama inavyoonyeshwa katika mchoro hapa chini. Kumekuwepo na ongezeko la idadi na kasi ya usajili wa namba za simu kati ya mwezi Julai na Desemba 2009, kutoka 842, 835 zilizosailiwa mwezi Julai hadi 6,378, 643 kufikia 20 Desemba 2009.



4. Ikumbukwe pia kuwa idadi ya namba za simu nchini imekuwa ikiongezeka maradufu nchini katika miaka ya hivi karibuni kama inavyoonyeshwa kwenye mchoro hapa chini. Idadi imeongezeka kutoka 284,109 mwaka 2000 hadi kufikia 14 903 024 mwaka huu wa 2009. Ikilinganishwa na idadi ya namba zilizosajiliwa, yaani 6 378 643 ina maana asilimia 43% ndiyo zimeshasajiliwa.



5. Ingawa zoezi la kusajili namba za simu limeendelea vyema katika miezi sita iliyopita, kumekuwepo na changamoto nyingi kwa mfano uandikishaji katika sehemu za vijijini, uhakiki wa kutambulikana, ukosefu wa umeme kwa ajili ya kutoa nakala vivuli vya vitambulisho, na kuingiza namba zilizosajiliwa katika "Database" za mitandao ya mawasiliano.

6. Kazi ya kuweka utaratibu wa kusajili namba za simu katika sheria bado inaendelea na ikikamilika itakuwa ni lazima kwa mtu yeyote anayemiliki namba ya simu kujisajili.
7. Katokana na tathmini iliyofanyika kwa kuzingatia maslahi ya watumiaji na watoa huduma na wadau wengine wote nchini, Mamlaka ya Mawasiliano imeongeza muda wa kusajili namba za simu kwa muda wa miezi sita mingine hadi tarehe **30 Juni 2010**.
8. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kuwashukuru wananchi wote na watoa huduma za mawasiliano kwa ushirikiano walioonyesha katika zoezi la usajili kwa miezi sita iliyopita, na inategemewa kwamba ushirikiano huu utaendelea katika muda huu ulioongezwa ili kukamilisha zoezi husika.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mkuu  
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**  
**28 Desemba 2009**